



Sauti Juu Ya Maji

*Sauti Ya Bwana
i juu ya maji:*

Zaburi 29:3a

Paul D. Norcross

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Sauti Juu Ya Maji

*Sauti ya Bwana juu ya maji:
Mungu wa utukufu alipiga radi:
Bwana yu juu ya maji mengi.
Zaburi 29:3*

Rev. Dr. Paul D. Norcross, CEEd, MEng, BTh, BS

*Tafsiri ya Kiswahili na
Mchungaji George C. Ndulesi, M.Div*

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

© Haki 2003 – Paul D. Norcross

Haki zote zimehifadhiwa. Kunakili maandishi kwa ajili ya matumizi ya binafsi au faida ya kibiashara hakuruhusiwi bila ya ruhusa ya maandishi kutoka kwa mwandishi. Nukuu fupi za sentensi chache kwa ajili ya matumizi yasiyo ya kibiashara ya mtu binafsi au kundi au kuangalia kitabu kunatiwa moyo na hakuhitaji ruhusa.

Maandiko yote yanatoka katika tafsiri ya King James ama siyo imeonyeshwa. Maandishi makubwa na alama za mabano kwenye ni mkazo wa mwandishi. Matumizi ya hali ya chini kwa rejea za kishetani ni ya makusudi; yeye yuko chini ya miguu ya wale wanaoongozwa na Roho wa Mungu aliye hai.

*Picha ya jalada na David A. Norcross
Tafsiri ya Kiswahili na Mchungaji George C. Ndulisi, M.Div*

ISBN : 0-9671353-5-4

Vitabu vingine vilivyoandikwa na Paul Norcross:

- *Dining At The Master's Table: Kujifunza Kusikia Sauti ya Mungu*
- *Succeeding In Spiritual Warfare: Masomo Kutoka Kitabu cha Yoshua*
- *Marriage Seminar: Jinsi ya Kutembea Katika Roho Katika Ndoa Yako*
- *Acts 29 Course: Jinsi ya Kutembea Katika Roho (Vol I, II, III)*
- *Breaking The Authority of The Bastard Curse: Kulirejesha Kusanyiko la Bwana*
- *In The Secret Place: Kukuza Uhusiano Wako wa Karibu na Mungu*
- *How Can I Get My Healing From God?: Funguo za Kupokea na Kutunza Uponyaji Wako Kutoka kwa Mungu.*
- *Five Keys To Deeper Intimacy With The Lord: Ujumbe Kwa ajili ya Bibi-arusi wa Kristo*

Kwa maelezo zaidi ili kupata maadhishi na utaratibu wa semina za moja kwa moja, tafadhali wasiliana nasi kwa:

Kingdom Faith Ministries
P.O.Box 725
Charlemont, MA 01339
USA

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Sauti Juu Ya Maji

Yaliyomo

1. **Kilio cha Mioyo yetu.....5**
2. **Ule Mto wa Uzima.....8**
3. **Sauti Yake i Juu ya Maji.....13**
4. **Msiache Chemchemi.....18**
5. **Nyumbani Mwa Baba Yangu.....25**
6. **Shauku Ya Moyo Wake.....35**
7. **Mwanakondoo Atawachunga.....39**

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Kilio cha Mioyo Yetu

Kisha akanionyesha mto wa maji ya uzima, wenye kung'aa kama bilauri, ukitoka katika kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana – Kondoo

Ufunuo 22:1

Kupitia kote katika Neno la Mungu lililoandikwa, maji yanaonekana sana yakielezea ukweli mkuu wa kiroho: uzima wa milele wa Mungu unatiririka kutoka penye kiti chake cha enzi kwenda kwa watu wake. Uzima wa yule ambaye amekuwepo siku zote, na atakuwepo siku zote anaendelea kuwapa uzima wale wanayoyaonea kiu maji haya, na wale wanaomjia ili kunywa.

Yanaonekana kufahamika? Maneno haya yanatukumbusha juu ya wale ambao Yesu alisema juu yao siku ile ya mwisho ya Sikukuu Kubwa Yerusalemu takribani miaka elfu mbili iliyopita:

Yohana 7:37-39

Hata siku ya mwisho, siku ile kubwa ya sikukuu, Yesu akasimama, akapaza sauti yake akisema, Mtu akiona kiu na aje kwangu anywe. Aniaminiye mimi kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake. (Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa)

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Maji haya ni nini, yanapatikanaje, na kwa nini ni ya lazima? Kwa nini Yesu aliwahimiza wasikilizaji wake kunywa maji haya ambayo yeye peke yake ndiye anayeyatoa? Kwa nini aliongelea ukweli huu huu kwa mwanamke Msamria penye kisima cha maji katika Yohana sura ya nne, na kulirudia tena mara mbili zaidi¹ katika kipindi cha zaidi ya nusu karne baadaye kwa Mtume Yohana kama alivyoandika kitabu cha Ufunuo? Ni kitu gani juu ya maji haya ambacho kiliukamta moyo wa mwanamke huyu pale kisimani?

Yohana 4:9-15

Basi yule mwanamke Msamaria akamwambia Imekuwaje wewe Myahudi kutaka maji kwangu, nami mwanamke Msamaria? Maana Wayahudi hawachangamani na Wasamaria

Yesu akajibu, akamwambia, Kama ungekuwa na karama ya Mungu, naye ni nani akuambaiaye, Nipe maji ninywe, ungalimwomba yeye naye angalikupa maji yaliyo hai

Yule mwanamke akamwambia, Bwana huna kitu cha kutekea, na kisima ni kirefu, basi umeyapata wapi hayo maji yaliyo hai?

Wewe u mkubwa kuliko baba yetu Yakobo aliyetupa kisima hiki, naye mwenyewe akanywa maji yake na wanawe pia na wanyama wake?

Yesu akajibu, akamwambia, Kila anywaye maji haya ataona kiu tena, walakini ye yote atakayekunywa maji yale nitakayompa mimi hataona kiu milele; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemichemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele

¹ Ufunuo 7:17 Kwa maana huyo Mwana-kondoo aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga, naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai na Mungu atawafuta machozi yote katika macho yao.

Ufunuo 22:17 Na Roho na Bibi-arusi wasema, Njoo. Naye asikiaye na aseme, Njoo. Naye mwenye kiu aje.

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Yule mwanamke akamwambia,Bwana unipe maji hayo,nisione kiu,wala nisije hapa kuteka.

Je kilio cha moyo wako ni kama hiki?Je moyo wako unatamani kunywa kutoka kwenye chemichemi ya maji yaliyo hai, ili ya kwamba usione kiu tena kamwe?Je umekwisha kuwa na ujuzi wa ladha ya maji haya ya kiroho katika mwendo wako wa Kikristo?

Uwe na uhakika kuwa Yesu alikuja kuwapa maji ya kiroho bure wale wote wanaotamani kuyapokea. Lakini kujua kwa mazoea tu juu ya maji yaliyo hai ya kiroho yanayobainishwa katika Maandiko hakutoshi ili kupokea, zaidi kuliko kujua tu juu ya maji kunavyompatia msafiri wa jangwani mwenye kiu kuweza kunywa. Lazima hasa tunywe toka chemichemi ya Bwana, siyo tu kutambua kwamba ipo.Tusije tukakosea-Chemichemi Ya Maji Yaliyo Hai si kitabu,kama ambavyo maji si glasi inayoyabeba.Maandiko yalitoka kwenye Chemichemi, ingawaje yenyewe si Chemichemi yenyewe.Yesu Kristo ndiye ile Chemichemi.Na waamini wanaojifunza kunywa kutoka kwenye chemichemi Yake hawataona kiu tena.

Kusudi la kitabu hiki ni kufundisha maana ya kunywa toka kwenye Chemichemi ya Maji Yaliyo Hai,Yesu Kristo.Ningetemani sisi wote tungekuwa na kiu kama yule mwanamke pale kisimani,aliyekuwa tayari kuuacha mtungu wake wa thamani wenye mchanganyikowa mafundisho tofauti ya imani, na kujifunza kufurahia kunywa toka kwenye kisima cha Yesu Kristo.

Bwana na aongeze kiu yetu siku zote za maisha yeti.Na tuweke kambi kwenye oasisi ya uwepo Wake,na kunywa toka kwenye chemichemi Yake kila siku. Na iwe kwetu *kisima cha maji yakibubukia uzima wa milele.*

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Ule Mto Wa Uzima

Tena itakuwa, kila kiumbe hai kisongamacho, kila mahali itakapofika mito hiyo kitaishi:

Ezekieli 47:9a

Zaburi 1:1-3

Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki, wala hakusimama katika njia ya wakosaji wala hakuketi barazani pa wenye mzaha.

Bali sheria ya BWANA ndiyo impendezayo; Na sheria yake huitafakari mchana na usiku.

Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji, uzaao matunda yake kwa majira yake, wala jani lake halinyauki; na kila alifanyalo litafanikiwa.

Wote tumeiona miti iliyopo kwenye kingo za mito. Ndiyo mikubwa zaidi, yenye nguvu zaidi, na izaayo sana kwa sababu nyepesi sana kwamba huwa haipungukiwi na maji ya kuitegemeza. Kama ambavyo maji ni ya lazima kwa maisha ya kimwili, ndiyo ilivyo kwa maisha ya kiroho ya mtu. Kukosekana kwa maji husababisha kudumaa kwa mimea. Kukosekana kwa maji ya kiroho kutoka kwenye Chemichemi Ya Maji Yaliyo Hai kunaleta athari ileile kwa kukua kiroho kwa maisha ya waamini. Ie sheria ya Mungu iliyoandikwa ilikuja kutoka kwenye kisima kilekile kama maneno ya kinabii: kwa ufunuo kama watu watakatifu wa Mungu walivyosema (na wakaandika) wakiongozwa na Roho Mtakatifu²

²*II Petro 1:20-21 Mkijua neno hili kwanza ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu.*

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Hawa wanaume na wanawake ambao mizizi yao daima ilichota kutoka kwenye chanzo cha Kimungu cha maji, Ile Chemichemi Ya Maji Yaliyo Hai, Ule Mto Wa Uzima. Mto huu kamwe haukauki.

Huu ni mto halisi. Upo. Mungu yu kati ya mto huu (Ufunuo 22:1; Ezeieli 47:9). Waamini wanapoyapata na kunywa kutoka kwenye chanzo hiki cha Kimungu cha maji, maisha yao yanafanikiwa kimuijiza. Waamini wengi wamekwisha chungulia utoaji wa Mungu ulio mkubwa hapo kabla, labda katika matukio kadhaa. Lakini tuntaka tukae mahali hapa, na kuendelea kunywa toka chanzo Chake. Mioyo inapumua kwa kutosheka katika uwepo Wake katika oasisi ambayo haijui maelezo ya kutosheleza, lakini huchochea sifa zetu, na mshangao wetu wa furaha katika heshima yetu ya ukuu Wake na ya upendo kwetu. Mahali hapa, kuna mto wa wema, na neema, nguvu na amani, ujasiri na ushirika pamoja na Muumba wetu ambaye anatamani kukaa kati ya watu Wake.

Zaburi 46:1-5

Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu Msaada utakaonekana tele wakati wa mateso.

Kwa hiyo hatutaogopa, ijapobadilika nchi, Ijapotetemeka milimani moyoni mwa bahari;

Maji yake yajapovuma na kuumuka, ijapopepesuka kwa kiburi chake. Sela

Kuna mto, vijito vyake vyaufurahisha mji wa Mungu, Patakatifu pa maskani zake Aliye juu

Mungu yu katikati yake; hautatetemeshwa; Mungu atausaidia asubuhi na mapema.

Ule mto wa Mungu ndipo mahali ambapo kila mkristo anatamani kupandwa. Ni mahali ambapo si pa mafanikio na

Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu baali wanadamu walinena yaliotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

kuburudishwa tu bali ni pa uponyaji pia. Mungu atatuongoza kwenda kwenye mto huu,ndipo mahali ambapo nafsi zetu zinahuishwa.

Zaburi 36:8

Watahibishwa kwa unono wa nyumba yako:Nawe utawanyweshwa mto wa furaha zako

Zaburi 23:1-3

BWANA ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu katika malisho ya majani mabichi hunilaza:kando ya maji ya utulivu huniongoza:Hunihuisha nafsi na kuniongoza katika njia za haki kwa ajili ya jina lake.

Maji yaliyo hai,aina ya yale yanayotajwa hadi sasa (na maneno kama mto wa Mungu,maji ya utulivu, na Chemichemi Ya Maji Yaliyo Hai) yote yanatokana na chumba cha kiti cha enzi cha Mungu. Zingatia kuwa katika Ezekieli maji haya yanatiririka kutoka kwenye hekalu la kiti cha enzi cha Mungu..

Ezekieli 47:1-12

Baadaye akanileta tena mpaka lango la nyumba ,maji yalitoka chini ya kizingiti cha nyumba,kwa njia ya mashariki maana upande wa mbele wa nyumba ulielekea upande wa mashariki,nayo maji yakashuka toka chini ya upande wa kuume wa nyumba,upande wa kusini wa madhabahu

Ndipo akanileta nje kwa njia ya lango upande wa kaskazini,akanizungusha kwa njia ya nje mpaka lango la nje,kwa njia yake iliyoelekea mashariki; na tazama,maji yalitoka upande wa kuume.

Na alipotoka mtu yule,mwenye uzi wa kupimia mkononi mwake,kwenda masharikini, akapima dhiraa elfu,akanivusha maji yale;maji yakafika mpaka viweko vya miguu.Kisha akapima dhiraa elfu,akanivusha maji yale yakafika mpaka magotini.Kisha akapima dhiraa elfu,akanivusha maji maji yakafika mpaka viuno.

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Kisha akapima dhiraa elfu,yakawa mto nisioweza kuuvuka :maana maji yamezidi,maji ya kuogelea,mto usiovukika.

Akaniambia, Mwanadamu,je umeona haya?Kisha akanichukua akanirudisha mpaka ukingo wa mto.

Basi nikiisha kurudi, tazama,kando ya kingo wa mtoilikuwapo miti mingi sana,upande huu na upande huu.

Ndipo akaniambia,Maji haya yanatoka kwenda pande za nchi ya mashariki,nayo yanashuka mpaka Araba,na kuingia katika bahari;maji yatokezwayo yataingia baharini,na majiyake yataponyeka.

Tena itakuwa,kila kiumbe hai kisongamanacho,kila mahali itakapofika mito hiyo,kitaishi kutakuwepo wingi mkubwa wa samaki,kwa sababu maji haya yamefika huko maana maji yale yataponyeka, na kila kitu kitaishi po pote utakapofikilia mto huo. . .

Tena itakuwa, wavuvi watasimama karibu nao;toka Engedi mpaka En-eglamu,patakuwa mahali pa kutandazia nyavu;samaki wao watakuwa wa namna zao mbalimbali,kama samaki wa bahari kubwa,wengi sana.Bali mahali penye matope, na maziwa yake,hayataponywa;yataachwa yawe ya chumvi.

Na karibu na mto,juu ya ukingo wake,upande huu na upande huu,utamea kila mti wa chakula,ambao majani yake hayatanyauka, wala matunda yake hayatatindika kamwe;uttoa matunda mapya kila mwezi, kwa sababu maji yake yanatoka mahali patatifu; na na matunda yatakuwa ni chakula; na majani yake yatakuwa ni dawa

Zingatia kwamba uponyaji huu,maji ya kutegemeza hutiririka kutoka mahali patakatifu,nyumba ya Mungu.Waebrania 8:2 Yesu ndiye mhudumu wa mahali hapa pa patakatifu.Yesu Kristo huhudumu daima katika mahali ambapo maji ya kutegemeza maisha hutokea.Tena tunaona kina cha kilio Chake siku ya mwisho ya sikukuu kwa wenye kiu waje mahali hapo na kunywa maji:

Yohana 7:37-39

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

*Hata siku ya mwisho, siku ile kubwa ya sikukuu, Yesu akasimama, akapaza sauti yake akisema, **Mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe***

*Aniaminiye mimi, kama maandiko yalivyonena, **mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake.***

(Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; Kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa.)

Halafu, maji haya ni nini? Tunaweza kuona yale ambayo yanafanya katika maisha ya mwamini. Tunaweza kuona ile shauku ya Bwana wetu ya kutuhimiza kuyanywa. Tunaweza kuona yale ambayo linasema yanamhusu Roho Mtakatifu. Lakini yananywewa namna gani? Tutawezaje kuyapata sisi wenyewe?

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

§ Sura ya Tatu §

Sauti Yake I Juu Ya Maji

Sauti ya BWANA i juu ya maji: Mungu wa utukufu alipiga radi: BWANA yu juu ya maji mengi.

Zaburi 29:3

Mtiririko wa maji kutoka kwenye chumba cha kiti cha enzi cha Mungu ni mfano wa ajili ya sauti ya Bwana. Tulisoma katika sura iliyopita katika Zaburi 46:5 kwamba Mungu yu katikati ya maji haya. Suti yake inatembea juu ya maji haya (Zaburi 29:3), ikibebwa na Roho Mtakatifu yule yule aliyetulia juu ya maji, akingojea sauti yake kutamka dunia iwe katika Mwanzo sura ya kwanza. Sauti yake iliunda na bado inaendelea kuitegemeza dunia.³

³ *Waebrania 11:3 Kwa imani twafahamu ya kuwa **ulimwengu uliumbwa kwa neno** [yaani sauti iliyozungumza – **rhema**] la Mungu, ili ya kwamba hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyodhahiri.*

*Waebrania 1:3 Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, **alivichukua** [yaani akivitegemeza] **vitu vyote kwa amri** [neno la Kiyunani hapa ni **rhema**, maana yake neno lililozungumzwa yaani kwa sauti] **ya uweza wake**, akiisha kufanya utakaso wa dhambi aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu;*

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Leo, ni sauti ileile ya *rhema* ya Mungu, maneno ya *rhema* ya maji yaliyo hai yakitiririka kutoka katika chumba cha nyumba ya kiti chake cha enzi, ambayo waamini wanatakiwa wayasikie na kuishi kwayo⁴. Ni huu mtiririko wa mto wa maneno yaliyo kutoka kwenye chumba cha kiti chake cha enzi hadi kwenye roho ya kila mwamini ambao unajitokeza katika maandalizi ya kanisa, Bibi-arusi wa Kristo.

Waefeso 5:25-27

Enyi waume wapendeni wake zenu kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake

*Ili makusudi alitakase na **kulisafisha kwa maji katika Neno,***

Apate kujiletea Kanisa tukufu lisilo na ila wala kunyanzi, wala lo lote katika hayo, bali liwe takatifu lisilo na mawaa.

Ni ya muhimu namna gani mistari hii inakuwa kwa kadri tunavyoelewa jinsi Bibi-arusi wa Kristo anavyotakaswa, kuandaliwa, na kufanywa mtakatifu na bila mawaa kwa kusafishwa kwa maji kwa neno la ufunuo la *rhema*.

“Kwa neno” la Waefeso 5:26 ina maana ya moja kwa moja *en rhema*, maana yake “katika pumziko au kuendelea katika maneno yanayotamkwa”. Matamshi haya, maneno kutoka kwa Yesu, yanatoka kwake kwa njia ya Roho Mtakatifu, kama yale ambayo Yohana alipokea ili kuandika kitabu cha Ufunuo. Yanatokea katika kijito kilekile cha maji yaliyo hali ambayo Paulo alipokea alipokuwa akiandika Maandiko ya Agano Jipya ambayo aliyatangaza:

Kwa maana, ndugu zangu, injili hiyo niliyowahubiri, nawajulisha yakuwa si ya namna ya kibinadamu. Kwa kuwa

⁴*Mathayo 4:4 Naye akajibu akasema, Imeandikwa, mtu hataishi kwa mkate tu ila kwa kila neno [rhema neno lililotamkwa] litokalo katika kinywa cha Mungu.*

Angalia pia Kumbukumbu la Torati 8:3 ambalo linanukuu mstari huu kama kusudi la msingi la kuzunguka kote jangwani!

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

*sikuipokea kwa mwanadamu wala sikufundishwa na mwanadamu bali kwa ufunuo wa yesu Kristo*⁵. Ule “ufunuo wa Yesu Kristo” ni kutoka kwenye maneno ya maji yaliyo hai ambayo yalitiririka kwa Paulo kutoka kwenye nyumba ya Kristo. Paulo aliandika, kama Yohana alivyoandika kama alivyoelekezwa katika Ufunuo sura ya kwanza. Nasi pia tunatakiwa kuwa katika pumziko na kuendelea katika mto wa maneno ambayo Yesu anazungumza kwetu kutoka moyoni Mwake hadi kwenye roho ya kila mwamini. Maneno haya ambayo kwayo tunatakiwa kuishi – manenon ya *rhema* ya Mathayo 4:4 yanayotoka kwenye kinywa cha Mungu.

Mara nyingi tunajaribiwa kufikiri kwamba mtume Yohana na Paulo wako tofauti kipekee au wana sifa zaidi kuliko sisi tunapofanyika kondoo ambao husikia sauti ya Bwana (Yohana 10:17). Lakini kamwe hili siyo somo lote tunalojifunza kutoka katika Maandiko. Tunatakiwa kunywa kutoka katika kisima kilekile na neno hili la *rhema* kutoka Chemchemi ya Maji Yaliyo Hai, Maji ambayo hutusafisha na kutufanya tusiwe na doa au kunyanzi au au mawaa mbele yake ni jinsi tunavyokuwa tumejitayarisha kwa ajili ya arusi ya Bwana na Bibi-arusi. Kila mmoja ambaye ni wa kweli ataisikia sauti yake⁶, na *Yeye ambaye ni wa Mungu husikia maneno ya Mungu* [rhema]⁷ haya yalikuwa ni maneno ya Yesu kwa Pilato na wa Yuda waliomkataa mara alipoyasema maneno haya.

Muwe na uhakika, Ndugu, hatujamkataa Yeye tunapomkiri kama Bwana na Mwokozi wetu.

Warumi 10:8-11, 17

Lakini yanenaje? Lile neno [rhema] li karibu nawe, katika kinywa chako na katika moyo wako yaani ni lile neno [rhema] la imani tulihubililo. Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni

⁵ Wagalatia 1:11-12

⁶ Yohana 18:37

⁷ Yohana 8:47a

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, taokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu. Kwa maana andiko lanena, kila amwaminiye hatatayarika. Basi imani, chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa neno [rhema] la Mungu.

Wakati tunaweza kuhakikishiwa juu ya wokovu wetu, tusithubutu kujiingiza katika furaha na kukubaliana na msimamo mwingine. Lazima tuwemo kazini mwa Baba yetu, tukisonga mbele kwa mambo ya Roho Mtakatifu:

- ◆ Kujifunza kumpenda mpenzi wetu wa Kwanza Yesu Kristo (Ufunuo 2:1-7),
- ◆ Kuitengeneza mioyo yetu kuweza kusikia hata minong'ono Yake midogo (Wimbo ulio bora 2:14; 8:13-14; Waebrania 4:1-16; 12:25-29),
- ◆ Kujifunza kuishi kwa kila neno la ufunuo la maana *rhema* linalotoka kinywani Mwake (Mathayo 4:4; Kumbukumbu la Torati 8:3),
- ◆ Kuruhusu kwamba ufunuo ule wa *rhema* kutusafisha kiroho tuwe safi (Waefeso 5:26) na kujenga imani yetu (Warumi 10:17),
- ◆ Na kutulinda kutokana na uasi, dhambi, uchawi, ukaidi, uovu, ibada ya sanamu (1Samweli 15:22-23).

Haya ndiyo maandalizi yetu, kupitia kuoshwa katika mto wa neno lake *rhema* la uzima, kama Bibi-arusi asiye na doa, kunyanzi au mawaa. Je! Mpendwa wetu anaweza kumwoa Bibi-arusi ambaye hawezi kuongea naye, yule ambaye hajajifunza kuisikia sauti Yake, kwanza kama kondoo (Yohana 10), halafu kama mpenzi anayefurahishwa na uwepo wake (Wimbo ulio bora 2:14; na sura ya 1 na 2)? Huwa tuna kiu kwa ajili ay uwepo Wake, na hutamani kunywa kutoka kwenye kisima Chake, ile Chemchemi ya

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Uzima, kwa kusikia sauti ya Bwana, sauti ambayo hutembea juu ya maji yale matamu (Zaburi 46:4-5; 29:3-4; 36:8-12). Utukufu wa uwepo Wake hufunuliwa katika sauti Yake (Mwanzo 2:8; Kutoka 33:12-23; 1Samweli 3:21). Ni wa utukufu namna gani upendo wake na huruma yake kwetu, akituruhusu kumkaribia Yeye, na Yeye kutukaribia sisi!

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Msiache Chemchemi

Kwa maana watu hawa wametenda maovu mawili; wameniacha mimi niliye chemchemi ya maji ya uzima, wamejichimbia mabirika, mabirika yavujayo, yasiyoweza kuweka maji

Yermia 2:13

Tunaimarisha uhusiano wetu na Yeye kwa kadri tunavyokaribia, na kutumia muda peke yetu kwenye madhabahu tunayoyachagua kujiandaa katika miyo yetu. Kama Musa alivyokutana na Mungu mlangoni mwa Hema ya kukutania, hivyo kuna mahali poa kukutania tunapoandaa katika hema ya miyo yetu. Hapa ndipo mahali tunapojifunza kunywa kutoka Chemchemi ya Maji Yaliyo Hai.

Uovu mkubwa hutokea wakati watu wa Mungu wanaposhindwa kunywa kutoka kwenye Chemchemi hii, mahali pa kujifunzia kusikia sauti Yake. Kwanza, hawapokei yale maji ya lazima yanayotoa uzima wa milele ambayo yanahitajika kutegemeza maisha yao ya kiroho katika Bwana, wakiwa na hitaji kwa ajili la maji ya kiroho hata hivyo hugundua aina yao ya yale maji. Hii ndiyo maana kuna theolojia nyingi za kidini ulimwenguni kote, na hata nyingi ambazo zina yabia za ajabu zilizojengwa juu ya upendo. Lakini bado zinakosa kitu kimoja: Maji Yaliyo Hai.

Maji ya namna hiyo yanatoka kwenye chemchemi ya Yesu Kristo. Hii ndiyo maana dini kubwa za ulimwengu haziwezi kufanya miujiza ya Kristo ulimwenguni leo. Kwa masikitiko siyo Wakristo wengi ambao wanaweza kuifanya miujiza hiyo. Kwa nini iko hivi?

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Matunda mazuri hutoka kwenye miti mizuri ambayo inamwagiliwa vizuri. Maji Yaliyo Hai huzaa matunda yeye nguvu ya kiroho. Tunda la Maji Yaliyo Hai ni dhahiri. Waamini ambao hunywa kutoka Chemchemi ya Maji Yaliyo Hai wana tunda la Roho katika maisha yao. Tunda hili ni pamoja na uthibiisho wa Mungu juu ya huduma zao kwa ishara, miujiza na maajabu⁸. Kwa hakika hii ni pamoja na kuwaleta waliopotea. Lakini huduma halisi yaliyo hai kutoka kwa Yesu Kristo pia ni pamoja na miujiza, uponyaji, kutoa pepo, ishara za mtume, na ishara za Roho kama kunena kwa lugha.

⁸*Matendo 2:22 Enyi waume wa Israeli, sikilizeni maneno haya; Yesu wa Nazareti mtu aliyedhihirishwa na Mungu kwenu kwa miujiza na ajabu na ishara, ambazo Mungu alizifanya kwa mkono wake kati yenu kama ninyi wenyewe mnavyojua:*

Marko 17:17-20

Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; Kwa jina langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya; watahika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa nao watapata afya.

Baada ya kusema nao, alichukuliwa juu mbinguni akaketi mkono wa kuume wa Mungu.

Nao wale wakatoka wakihubiri kotekote, Bwana akitenda kazi pamoja na, kulithibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nao. Amen.

Yohana 14:12

Amini, Amini, Nawaambieni, yeye aniaminiye mimi kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam na kubwa kuliko hizo atafanya; kwa kuwa mimi naenda kwa Baba.

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Inafanya mtu kuwa makini kwa kutambua kwamba kwa sababu *Kwa kuwa mimi Bwana sina kigeugeu*⁹, hatuwezi kubadilisha njia ambayo Mungu huchagua kushughulika nasi. Tunahimizwa kunywa kutoka katika kisima Chake, na tunda la ufuatiliaji wa jinsi hiyo mara zote litajionyesha katika baraka Zake za kuthibitisha. Kama badala yake, tunafuata njia yetu wenyewe ya kufanya huduma, tukiendesha maisha yetu na huduma zetu bila ufunuo kutoka kwa Amiri-Jeshi wetu Mkuu, tutakuwa kama Kaini aliyefanya kwa kweli sehemu ya wajibu wake mbele za Mungu lakini aliufanya katika njia ambayo alifikiri ungefanyika badala ya njia ambayo Mungu alimwambia kwa ufunuo. Matokeo? Mungu hakuikubali sadaka yake. Kaini alimkasirikia Mungu. Kupitia hasira yenye wivu aliilekeza hasira yake dhadi ya ndugu yake mwenyewe na kumwua. Lazima tufanye matendo yetu ya kidini kupitia kusikia sauti ya Mungu na kuitii kikamilifu.

Ni huduma ngapi ambazo zinafanya kazi za ajabu namna hiyo (katika akili zao na zile za wafuasi wao) bado Mungu hajaonyesha uthibitisho wake wa dalili za kimiujiza wa ishara na maajabu? Rafiki zangu pasipokuwa na ufunuo kutoka kisima cha Yesu Kristo yaani mafundisho mengi ya Kikristo yenye majina mengi yanainuka, na kusababisha kujaan kwa ajenda za kanisa pamoja na shughuli nyingi. Lakini anakosa uthibitisho wa Mungu. Kumetokea nini?

Kama vile watu wa Mungu waliokufa jngwani kwa kushinda kusikia sauti ya Bwana¹⁰ vivyo hivyo Mungu

⁹Malaki 3:6

¹⁰ *Yoshua 5:6 Kwa kuwa wana wa Israeli walitembea muda wa miaka arobaini barani, hata hilo taifa zima, yaani, watu waume waendo vitani, waliotoka Misri, walipokuwa wameangamia kwa sababu hawakuisikiliza sauti ya BWANA [Kiebrania, "Shama" maana yake kusikia, kusikiliza, na kutii, kuelewa] nao ndiyo BWANA aliyewaapia ya kwamba hatawacha waione hiyo nchi, Ambayo BWANA aliwaapia baba zao kwamba atatupa sisi; nchi ijaayo maziwa na asali.*

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

ataruhusu watu wake kufa katika jangwa lao leo mpaka hatimaye watapojifunza kusikia na kutii sauti yake wao wenyewe, hivyo wakinywa kutoka kwenye Chemchemi ya Maji Yaliyo Hai, Yesu Kristo. Ndipo tu Bwana atakapowaruhusu kuvuka Yordani yao na kuingia katika Nchi ya Ahadi ya baraka za Agano Jipya. Mpaka hapo, Kanisa linabaki halina nguvu, dhaifu, lililochanganyikiwa, na lisilo na matunda kulinganisha na mwendo wa Kristo wenye nguvu ambao linatakiwa liwe nalo kama matokeo ya kusikia na kuitii sauti yake. Ni sauti hii inayotiririka kama maji ya uhai kutoka kwenye nyumba ya Mungu.

Mng'ao katika macho ya Yesu unaendelea kuwa kanisa Lake. Ni jinsi gani anavyofurahia kuwa na ushirika binafsi pamoja na Bibi-arusi Wake mzuri! Jinsi yeye (Bibi-arusi) anavyomtamani Yeye, Mpenzi Wake wa kwanza! Huu ndiyo moyo wa wale ambao Yesu anawaandaa kwa kuoshwa na maji na maneno Yake ya ufunuo yanayoendelea. Kutoka ndani yao wamejifunza kusikia mtiririko (*rheo* – msingi wa *rhema*) wa sauti kwenda kwenye roho zao (Yohana 7:37-39). Hii ndiyo njia ambayo kwayo anamwandaa kwa ajili ya siku yake ya arusi pamoja na Mfalme; akimsafisha kwa maji ya Roho Mtakatifu, akimfanya asiwe na doa au kunyanzi au mawaa.

Ufunuo 3:20-22

Tazama nasimama mlangoni nabisha, mtu akisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake na nitakula pamoja naye nay eye pamoja nami.

Yeye ashindi nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama ambavyo nami nilishinda, na nimekletishwa pamoja na Baba yangu katika kiti cha enzi.

Yeye aliye na sikio na asikie lile ambalo Roho anayaambia makanisa.

Kama Mfalme alivyonyoosha fimbo Yake kwa Malkia Esta, ili ya kwamba yeye aliandaliwa aingie katika uwepo wake, hivyo Bibi arusi wa Kristo leo anapewa haki ya kuingia katika uwepo wa Mfalme. Tunagusa moyo Wake kama Esta alivyougusa ule wa mume wake. Alisema kwanza, halafu

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

yeye Esta akajifunza kusikiliza. Alishinda na alikaribishwa kuketi pamoja na Mfalme kwenye kiti chake cha enzi. Je! waamini wote watakuwa tayari kusikia kutoka kwenye Chemchemi ya Maji Yaliyo Hai.

Je! maandalizi haya yanaanzishwa vipi? Kuna mifano mingi katika Maandiko. Mtume Paulo, kwa mfano, alienda arabuni kwa miaka mitatu, lakini haikuwa kujifunza Biblia. Alijua vizuri sana, kwa hivyo sisi tunatakiwa kujua pia. Kwa kweli ufunuo hauwezi kuthibitisha bila Maandiko. Lakini Paulo alikwenda ana arabuni siyo kujifunza Maandiko zaidi, bali kujifunza kusikia sauti ya Bwana. Alikwenda na kujifunza kuishi na kutembea na kuwa na uhai wake katika Yeye, kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu. Ilimchukua miaka mitatu.

Je! itatuchukua sisi muda mrefu hivyo? Hiyo inategemea. Je! utakuwa tayari kuwekeza miaka mitatu kama hivyo Bwana alikwambia ufanye? Uko tayari kuuza vyote na kununua hili shamba lililo na hazina ya ukaribu na Yeye, au wewe kama kijana tajiri aliyependa mali zake za dunia kuliko kumpenda Bwana, na hivyo asingeweza kuacha vyote na kumfuata Yeye? Hebu fikiriri uliahidiwa dola milioni kumi baada ya kumaliza maka mitatu ya mafunzo. Ungeweza kuacha kazi yako ya sasa hivi na kuwekeza katika miaka mitatu ya maisha yako? Kwa nini waamini hawaoni uwekezaji wao katika kujua sauti ya maji yaliyo hai ya Kristo katika njia hiyohiyo? Je! hazina zake si zina thamani zaidi sana?

Bwana ana mtaala binafsi uliotayarishwa kwa kila mwamini. Umetengenezwa kuwasaidia kutimiza kusudi lao walilopewa na Mungu **baada** ya kujifunza kunywa kutoka chemchemi yake ya maji yalio hai. Mitindo yetu ya maisha, shuhguli zetu, na

vipingamizi vyetu mara zote ni hazina tunazozing'ang'ania. Lakini pamoja navyo vikiwa mikononi mwetu, tunaweza kuwa kama yule kijana tajiri ambaye alikimbia kutoka kwenye kisima cha Uzima cha maji kwa

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

sababu ya gharama ya kufuata mtaala wa Bwana ambao ulikuwa mkubwa sana kwa ajili yake kuubeba.

Yesu kamwe hakutuambia tuigiza huduma ya mtu mwingine. Wazo hili ni mojawapo ya mizigo mizito ya ugunduzi wetu wa kidini. Tunadhani kwamba atatuambia tende upande mwingine wa ulimwengu au tuishi katika umaskini. Bwana anatuambia sisi kuisikia sauti yake na kuitii. Hivyo anacho kwamba wewe kitakuwa tofauti kuliko anavyoniambia mimi. Alimwambia Petro kutakuwa msikivu kuhusu aina ya huduma ambayo Yohana atakuwa nayo. Waamini wengine wanaogopa sana yasiyojulikana, na wanashikilia sana wanayoyajua, kiasi kwamba hataweza kumtumaini Bwana kuongoza mapito yao kwenda kwenye mapenzi ya Mungu kwa ajili ya maisha yao. Matokeo yao yanakosa ule mpango wa ki – Mungu wa ajabu, kusudi, matarajio na taji za kimbingu ambazo Mungu ameweka kwajaili yao kupokea! Yote haya kwa sababu kwa ujeuri hukataa, au kwa shingo upande tu haijalishi kwamba wanachukua muda wo wote wa lazima kujifunza kwa ujasiri kusikia na kwa moyo kutii sauti ya Bwana.

Wapendwa wengi ngugu na dada katika Kristo huomba kujua mapenzi ya Bwana, (maombi ambayo kwa wazi kabisa hayakon kwenye Biblia), lakini je! mtoto anahitaji kuomba kujua mapenzi ya wazazi wake ambao ana uhusiano wa karibu nao? Je! hawako mara zote kumfundisha, kumwongoza na kumwelekeza katika upendo? Ule uwekezaji ambao mtu anaufanya katika kujifunza kusikia na kutii sauti ya Mchungaji wetu itamlipa faida kubwa sana katika maisha haya na yale yajayo.

Watu wa Musa walikataa kwenda juu mlimani kuisikia sauti ya Bwana, bali walimchagua Musa kufanya kwa ajili yao¹¹. Ni jinsi gani Bwana atavutiwa na kanisa ambalo wanamwomba mchungaji wao kuwa sauti ya Mungu kwao?

¹¹ Waebrania 12:18-29

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

“Nifuate” Yesu alimwashiria Petro baada ya kukutana na moyo wa kumkana wa Petro katika Yohana 19:15-22. Maneno “nifuate” yanamaanisha kumfuata Yeye aliyetangulia, kuwa pamoja naye, kujiunga kama mtumishi¹². Yesu anatuambia kuwa kumwandama. Anatoa maji ya uzima kwa wale ambao kwa kweli wanachukua muda kutoka kwenye shughuli zao na kuchukua muda pamoja naye peke yao. Huwashirikisha moyo wake kwa upendo sana – tutaachaje kupendana naye kwa kadri anavyoongea na sisi njiani? Atawezaje kutupa maji matulivu, yeye kuburudisha yaliyo hai, kama hatutaka kujifunza kuja kwake?

Mahali pa maombi ni kwa ajili ya kuwasiliana na Yule ambaye siku zote anaishi kuwaombea watakatifu. Tunaweza kujifunza kumruhusu atupe ajenda kila siku. Mwenye kuianzisha na kuitimiza imani yetu husubiri wito wa nafsi yenye njaa ambayo inatamani kula mkate mpya wa ufunuo wa mana. Anabeba maji yaliyo hai kwa wote wenye kiu, na hayo maji peke yake yatakuwa chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele. Ni kwa jinsi gani upendo wake unatusukuma kwenda kwake tunapokuwa wadhaifu na ni kwa haraka jinsi gani anatutia nguvu kwa kadri tunavyojifunza kutulia katika uwepo wake kama Elia alivyojifunza kufanya¹³, kuingia rahani mwake, kupumzika kutoka kwa kazi zetu¹⁴, kumruhusu Yeye kufanya kazi Yake. Kamwe tusiiache chemchemi, na kuridhika kwa ajili ya mawasiliano ya upande mmoja tu na Mwalimu Mkuu.

¹² Itifaki ya Strong, *akoloutheo* # 190

¹³ 1Wafalme 19:12

¹⁴ Wabrania 4:9-11

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Nyumbani Mwa Baba Yangu

Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi: kama sivyoy, ningaliwaambia.Maana ninaenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali nitakuja tena, niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi nanyi muwepo.
Yohana 14:2-3

Ni furaha iliyoje kuketi katika bustani pamoja na Mpendwa wetu, Bwana Yesu Kristo, ambaye hamu yake kubwa ni kumfundisha kila mmoja wetu jinsi ya kuingia na kupumzika katika chumba cha kiti cha enzi cha uwepo wa Mungu. “Ili wawe na umoja kama sisi tulivyo umoja” aliomba Yesu bustanini katika Yohana 17:22.

Ninaamini ile shauku katika kila roho ni kuwa umoja na Mungu.Hii ni hamu ambayo inatakiwa ipaliliwe.Yesu Kristo alikuja kufanya “umoja” uwe uhalisi kwa ajili ya hao wanaotamani kwenda huko!

Katika Yohana 14, Bwana anatoa usemi wa ajabu kuhusu maisha yetu ya wakati ujao:

Yohana 14:1-2

Msifadhaike mioyoni mwenu: mnamwamini Mungu, niaminini na mimi.

Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi, kama sivyoy ningaliwaambia.Maana naenda kuwaandalia mahali.

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Mara ngapi nimeshaisoma mistari hii na nimefarijika kufiki juu ya makao ya wakati ujao yaliyoandaliwa kwa ajili yangu tu mbinguni. Ni rahisi kufikiri juu ya vitu vya anasa ambavyo tungependa kuwa navyo huko. Labda hii ni picha ya mbinguni ya wakati ujao kwa ajili yetu. Lakini siku moja nilivyokuwa nikisoma mistari hii, Bwana alianza kunionyesha kweli fulani ambazo zilivuta usikivu wangu.

Neno “makao” linatafsiriwa vizuri zaidi “mahali pa kuishi” au “makao”. Kwa kadri nilivyotafakari mistari hii Roho Mtakatifu alianza kunionyesha kwamba mistari hii kwa urahisi haizungumzii mahali pa wakati ujao. Tafakari mistari wa 3:

Yohana 14:3

Basi nikienda na kuwaandalia mahali nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi nanyi muwepo.

Ufunguo wa kuelewa mistari hii uko katika kutambua kwamba Yesu anazungumza kwa Roho Mtakatifu juu ya mahali katika Roho mahali nilipo. Hasemi “mahali nilipokuwa” au “mahali nitakapokuwepo”, bali “mahali nilipo.” Kwa maneno mengine, mahali Yesu alipo sasa unaweza kuwepo pale pia. Hapo ni mahali katika Roho, siyo mahali pa kimwili.

Yesu alihitaji kuondoka ili amruhusu Mfariji, Roho Mtakatifu kuja (Yoh 16:7). Moja wapo ya makusudi ya Yesu kuondoka ilikuwa ni kuandaa mahali katika Roho kwa ajili yako kukaa ndani yake, ili kwamba uweze kuwa mahali Yesu Kristo alipo.

Unaweza kuwa unafikiria, “Ah, nilifikiri kufuatana na Wakolosai 1:26-27 kwamba ni Kristo ndani yangu, tumaini la utukufu,” na uko sahihi. Kristo hasa yuko ndani ya kila mwanini aliyezaliwa mara ya pili. Lakini elewa hili – mahali tunapokutana na Yesu ni mahali pa kiroho mahali pa ukaribu na ushirika pamoja na Baba na pamoja na Yesu Kristo ni mahali katika Roho. Yesu alienda kuaandaa mahali

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

hapo kwa ajili yako ili uweze kwenda pale wakati wo wote unapotaka.

Daudi alipaita mahali hapa “mahali pa siri pake Aliye juu” katika Zburi 91:1. Yohana aliparejea mahali hapa kama mahali pa kula pamoja na Bwana mezani Pake (Ufunuo 3:20). Hakuna ye yote ambaye alikwisha kufurahia kutembea kwa karibu kwa binafsi pamoja na Bwana na akafanya makuu kwa ajili ya Ufalme aliyeshindwa kuelewa na kutekeleza ukweli huu wa kiroho: Kwamba wewe na mimi tuliumba kwa ajili ya ushirika wa karibu na Yesu Kristo, na kupitia kwake ushirika wa karibu pamoja na Baba hii ndiyo sababu Yesu alikuja na kufa kwa ajili yako. Kutembea katika Roho kunategemea kunategemea juu ya kujifunza kuingia mahalia hapa pa uhusiano wa karibu na Yesu.

Sauti Kutoka Wakati uliopita

Ngoja nikushirikishe kitu kutoka kwenye kitabu changu ninachokipenda, Kumuiga Kristo .Kiliandikwa na mtawa aliyeitwa Thomas a’ Kempis, ambaye aliandika mwanzoni mwa miaka ya 1400. Makala iliyoitwa “Of the Inward Speaking of Christ to a Faithfull Soul” aliandika:

Nitachukua tahadhari, inasema roho iliyojitoa na nitasikia kile ambacho Bwana wangu Yesu ataniambia. Heri ni mtu yule asikiaye Yesu akizungumza katika roho yake, na anayechukua kutoka mdomoni mwake maneno fulani ya faraja¹⁵. Heri masikio yale yanayosikia minang’ono ya siri ya Yesu, na kutochukua tahadhari yo yote kwa minong’ono ya udanganyifu ya ulimwengu huu, na heri masikio yale mazuri laini ambayo hayachukui tahadhari kwa sauti za nje bali kwa

¹⁵ Mathayo 4:4 – Mtu hataishi kwa mkate tu bali kwa kila neno (rhema – yaani mana ya ufunuo) linalotoka katika kinywa cha Mungu.

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God’s People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Mungu anasema na kufundisha katika roho¹⁶. Yamebarikiwa macho yale yaliyofungwa kwa muonekano wa ubatili wa nje na kuchukua tahadhari kwa mienendo ya ndani ya Mungu. Heri ni wale pia, wanaopata wema na kujiandaa kwa kazi za mwili na za kiroho ili kupokea kila siku siri za uvuvio na mafundisho ya ndani ya Mungu. na Heri ni wale wanaojitoa kikamilifu kumtumikia Mungu na wale ambiao kwa ajili ya huduma yake wanaweka mbali viziwizi vyote vya ulimwengu.

Eh! Nafsi yangu usijali yale yaliyosemwa kabla na funga milangon ya ufahamu ambazo ni njia tano za fahamu, ili ya kwamba uweze kusikia kwa ndani lile ambalo Bwana Yesu anazungumza ndani ya nafsi yako. Hivi ndivyo asemavyo Mpenzi wako: Mimi ni afya yako, Mimi ni amani yako, Mimi ni uzima wako. Dumu ndani yangu na utapatya amani ndani yanguacha upendo wa vitu vinavyopita na tafuta vitu ambavyo ni vya milele. Ni vitu gani vya muda laniki ni vya udanganyifu? Na kiumbe cho chote kinaweza nini kwako kama Bwana Yesu akikuacha? Kwa hiyo, kuacha na kutengana na viumbe vyote na mambo yote ya ulimwengu, fanya kile kilicho ndani yako ili ujifanye wa kupendeza machoni pake, ili uweze baada ya maisha haya kuja kwenye uzima wa milele katika ufalme wa mbinguni¹⁷.

Yesu alienda kutayarisha mahali hapa pa kusikia sauti yake, mahali ambapo tunaweza kujifunza kuishi kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu. Kondoo Wake huisikia sauti yake, na kumfuata. Hawafuati sauti ya mwingine. Kuongozwa na Roho ni kuongozwa na kwa shauri la Yesu, kushirikiana na kanisa lake moja kwa moja. “Mkikaa ndani yangu na maneno yangu yakikaa ndani yenu....” inazungumza juu ya Yohana 15:7. Je uhusiano na

¹⁶ 1 Yohana 2:27 – Nanyi, mafuta yale mliyoyapata kwake yanakaa ndani yenu, wala hamna haja ya mtu kuwa fundisha lakini kama mafuta yake yanavyowafundisha habari ya mambo yote, tena ni kweli wala si uongo, na kama yalivyowafundisha kaendi ndani yake

¹⁷ á Kempis, Thomas; *The Imitation of Christ*; Doubleday, 1985

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

mtu fulani unayempenda unaweza kujengwa tu juu ya yale yaliyoandikwa **juu** yake, badala ya mawasiliano halisi **pamoja** naye? Ni furaha iliyoje katika kusikia sauti ya Bwana-arusi! Kila siku ni tukio jipya pamoja na yule umpendaye, Yesu Kristo.

Ufalme wa Mungu ni Uwepo Wake

Maana ufalme wa Mungu si kunywa wala kula, bali ni haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu¹⁸.Ufalme wa Mungu.Maana ufalme wa Mungu hauwi katika neno, bali katika nguvu¹⁹, ufalme wa kuchunguza (yaani kwa milango mitano ya fahamu)lakini umo ndani yenu²⁰.

Ufalme wa Mungu siyo mahali na siyo kipindi cha wakati.Badala yake ni uwepo wa Mungu.Ni uwepo wa Mungu tunaoutafuta kwanza, na haki Yake, hayo yote (yanayohitajikwa katika maisha haya) mtazidishiwa²¹.Ni uwepo wa Mungu ambao unakuja kwa kadri tunavyojenga uhusiano binafsi pamoja na Yesu Kristo ambao unatosheleza hamu ya kila mmoja.Yeye anatakiwa mapigo yetu ya moyo! Kama ile hamu kubwa ya mwanamke Mshunami ya kuwa pamoja na kijana wake mchunga kondoo katika kitabu cha Wimbo Ulio Bora, hivyo na sisi tutakua kumtamani Yeye tunayempenda, Yesu Kristo.

Endelea kuwa na njaa kwa ajili yake kwa kutumia muda kumtafuta Yeye kila siku.Ataonekana kwa wale wote wanaomtafuta.

¹⁸ Warumi 14:17

¹⁹ 1Wakorintho 4:20

²⁰ Luka 17:20-21

²¹ Mathayo 6:33

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Kumtambua Yeye

Nilikuwa nikilia kwa Mungu kila niliposoma Mithali 3:5-6. Ningeomba, “Mungu hata kama ni mara moja tu katika maisha yangu ningeweza kuitendea kazi mistari hii, ningekuwa na shukrani sana.” Halafu nikakutana na Yesu, na nikaanza kutambua jinsi ilivyo rahisi hasa kuitendea kazi mistahi hii. Inaweza kuwa rahisi kama kupumua:

Mithali 3:5-6

Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote: wala usitegemee akili zako mwenyewe.

Katika njia zako zote mkiri Yeye, naye atanyosha mapito yako.

Bwana alitumia mfano kunifundisha miatari hii. Alinionyesha picha ya daraja lenye ngazi tatu. Mjini New York kwa mfano, kuna madaraja ambayo yana barabara kuu mbili, moja juu ya nyingine. Kutoka kwenye barabara ya chini unaweza kuangalia juu kuona kinachoonekana kama dari au paa juu yako, na hutaweza kujua kama kuna barabara nyingine kamili juu yake kama hujui vinginevyo. Bwana alikuwa ananionyesha kwamba wanaume na wanawake wanaweza kusafiri kwenye barabara kuu ya chini na wakaendesha na miili yao pamoja na tamaa na matakwa yake au wanaweza kusafiri kwenye ngazi ya katikati juu ya barabara ya nfsi zao (mahali ambapo panakaa haiba ya mtu, mawazo ya kibinadamu, hisia na kufikiri). Lakini yanye faida zaidi wanaweza wakasafiri kwenye ngazi ya juu zaidi kuliko zote, barabara ya Roho. Barabara kuu ya ulimwengu wa Roho juu ya nfsi na mwili, na kutoka kwenye njia yo yote kutoka kwenye zile barabara mbili za chini, ni vigumu kusema kwamba hata iko barabara nyingine kuu ya Roho yako.

Halafu Bwana akanionyesha kwamba njia ya kuingia kwenye njia kuu ya Roho ni kwa urahisi tu kumtambua Yeye katika njia zako zote siku nzima. Tunaposimama kwa muda kutoka katika shughuli zetu na kumtambua Yeye,

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

tunaweza kuruka mpaka kwenye njia kuu ya Ki-roho. Na kusafiri juu yake. Na kusafiri kwa kuishi katika Roho ni furaha zaidi kuliko kusafiri kwenye ngazi ya nafsi zetu ai miili yatu? Kumtambua Bwana kunatuwezesha kuingia katika mambo ya Roho. Hii ndiyo njia ambayo Munguamekusudia tuishi kwayo. Kama utatamani kuishi katika ulimwengu wa miujiza, mtambue Yeye, na ujifunze kusikiliza sauti yake ndogo nay a utulivu ambayo itanyosha mapito yako.

Ngoja niwashirikishe mfano wa karibuni wa jambo lililotokea nilipokuwa nikirudi kutoka kwenye safari ya umisheni Romania. Nikiwa pamoja na ndugu Carl Fox na timu ya wahudumu wa ajabu, tulitumia wiki tatu kufundisha katika makanisa na kufanya uinjilisti katika mitaa na vijiji pamoja na watakatifu wa ajabu.

Nikiwa njiani narudi nyumbani, nilisimama kwa muda London kumtembelea mwamini wa ajabu ambaye alikuwa amefurahia kitabu changu cha Dining at the Master's Table: Kujifunza kusikia sauti ya Bwana, halikadhalika kitabu cha mchungaji Carl Fox Turning Curses To Blessings.²² Baada ya muda mzuri wa ushirika, yule mwamini alinipeleka uwanja wa ndege kwa ajili ya kurudi nyumbani Boston.

Niliingia kwenye Bustani ya wanyama pale uwanja wa ndege wa Heathrow. Uwanja ulikuwa umejaa maelfu ya watu walio na hasira ambao safari zao zilikuwa zimefutwa. Ilitokea kwamba ziku ile viwanja vikuu vya ndege vya Ulaya vilikwisha kuamua kubadilisha usimamizi wa ndege kwenye kompyuta mpya. Safari nyingi zilikuwa zinafutwa kwa ababu mfumo wa kubadilisha ulishindwa kufanya kazi. Sasa ningeweza kukaa London siku kadhaa na kuona jinsi nitakavyobarikiwa! Lakini pasipo kusaidiwa gharama na mashirika ya ndege nisingeweza kwa sababu

²² Vitabu vyote viwili ni vya msaada kwa kujifunza funguo za utendaji wa kuongeza ujasiri katika kuisikia sauti ya Bwana. Wasiliana na Huduma ya Kngdomfaith, ambayo imeonyeshwa nyuma ya kitabu hiki, kwa ajili ya habari zaidi.

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

nilikweisha kutoa karibu fedha zangu zote kusaidia waamini katika Romania.Kwa sababu tatizo lilikuwa la kiseriakali, hakuna shirika la ndege lingeweza kusaidia kulipa hizo gharama za zaidi.Hasira ya lile kundi ilikuwa juu ya ukweli kwamba mashirika yalikuwa yanasema yasingeweza kupanga tena safari kwa siku nyingine nne au tano zaidi!

Ilinichukua saa moja kukaa katika mstari wa maelfu ya watu ili kutambua nilihitaji kufanya zaidi ya kusimama tu kwenye mstari.Nikaanza kutembea hapa na pale katika jingo, nikiimba kwa lugha.Nilianza kumsifu Mungu kwa Yeye kuwa katika utawala.Nilimsifu Yeye kwamba alijua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu kwamba tatizo hili lingetokea.Nilimpigia simu mke wangu wa ajabu Ritha na nikamwomba kuwaambia vikundi cha maombezi waombe.Nilikuwa naanza kumtumaini Mungu wa moyo wangu wote.Na kutotegemea akili zangu mwenyewe.Na kama nilivyoendelea kumtambua, aliyanyosha mapito yangu.

Wazo likaja kwa kadri nilivyokuwa nasifu kwenda na kuongea na wakala wa tikiti.Nilijua katika roho yangu kwamba wazo hili lilitoka kwa Mungu.Ile mistari ya kukata tikiti ilikuwa haipo kwa sababu wasafiri wote waliokata tamaa walikuwa wanasimama katika sehemu ya kuhudumia wasafiri wakipiaga kelele kwa wale mawakala.

Yule wakala wa kuakata tikiti aliniambia angeweza kuniweka mimi kwenye kungojea kwa ajili ya safari moja tu ambayo ilikuwa haijafutwa ya kwenda Boston.Lakini ningekuwa mtu wa 30 katika watu wanaosubiri.Kulikuwa na tumaini dogo kwa ajili ya safari ambayo mamia walitarajia kuingia kwenye ndege.Nilisubiri masaa matatu yaliyobakia ya maombezi, kila wakati nilikuwa naimba sifa kwa Mungu katika lile jengo.Katika kipindi kile, Bwana aliniambia kwa ahakika ningeweza kupata nafasi katika ndege hiyo.Haleluya! Sasa nilikuwa na ufunuo wa hakia wa *rhema* neno ambalo ningeweza kushikilia, na pamoja na

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Mungu nimejifunza kwamba hakuna neno la *rhema* ambalo haliwezekani (Luka 1:37).

Mwishowe muda ulifika wa kuonekana kwenye kaunta sahihi kwa ajili ya kungjea wito. Nilikuwa nimekwisha tu nimemaliza kujibu swali kutoka kwa mwanamke aliyesimama karibu nami, ambaye alikuwa namba 28 kwenye orodha ya kungojea. Nilikuwa nikimshuhudia habari za Kristo, na alikuwa tu ametoka kuniuliza, “natumaini umekuwa ukiombea safari hii?” Nilimwakishishia kwamba nilikuwa naomba, na mara ile yule wakala wa tikiti akaanza kuita majina. Na sasa ilikuwa dakika 15 kabla ya ndege kuondoka, na lango la kuingilia kwenye ndege lilikuwa mbali kutoka kwenye kaunta. Yule wakala akaita jina la kwanza, jina lilifuta lilikuwa langu! Badala ya namba 30 kwa namna fulani Mungu alikuwa amebadilisha mpaka namba 2!

Nilikimbia kwenda kwenye ndege na nikaketi mara moja kwenye kiti changu. Dakika chache baadaye, mtu mwingine akakimbia tena akakimbia kuingia kwenye ndege na akakaa karibu na mimi. Masaa mawili mawili yaliyofuata yalikuwa ni masaa ya furaha ya kushudia habari za Yesu Kristo kwa mtu huyu, ambaye aliniambia baadaye aliniambia jinsi alivyofurahia kusikia juu ya Bwana. Na jinsi kwa kawaida huchukia kuzungumza kwenye ndege, na kwa makusudi kamwe huwa hazungumzi na mtu ye yote! Alikuwa ameokoka, lakini alikuwa kamwe hajawahi kuona jinsi Mungu alivyomtaka yeye kujifunza kumkaribia, ili aweze kusikia sauti yake na kuwa na ushirika naye.

Unaona, Mungu yuko tayari kutembea kwa Roho. Anatamani sana kuongoza hatua zetu tunapomkiri Yeye katika njia zetu zote. Furaha yetu ni kuruhusu nia hii iwe ndani yetu ambayo pia ilikuwa katika Kristo Yesu²³, na tujifunze kuwa katika njia kuu ya Roho wa Mungu badala ya barabara ya miili yetu na nafsi zetu za kidunia. Yesu alienda kuandaa mahali hapa kwa ajili yetu na kwenda na

²³ Wafilipi 2:5

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

kudumu. Alifanya hivyo ili tuweze kupata kupajua mahali hapa **leo**.

Hakuna furaha iliyo kubwa zaidi kuliko kutembea kila wakati katika ushirika na Yesu Kristo na pamoja na Baba. Unapendwa na unakaribishwa kutumia muda katika uwepo wa Mfalme. Unakaribishwa kumruhusu kukuongoza kando ya maji ya utulivu, mahali ambapo anaihuisha nafsi yako. Yule mtu tajiri hakuweza kuweka kando kilishokuwa cha thamani katika maisha yake, bali alitaka kukishikilia. Haupti muda mrefu baada ya kupendana na Yesu Kristo ambapo tunagundua jinsi ilivyo ndogo nafasi ya vitu vya maisha haya kwetu. Kama yule mtu aliyejifunza juu ya hazina katika shamba, na alikuwa tayari kuuza vyote kulinunua lile shamba, hivyo tuna hazina ya namna hiyo katika uhusiano wetu na Yesu Kristo, kwamba tuko tayari kufanya lo lote tuwezalo katika shughuli za maisha yetu kutumia muda zaidi pamoja na Mpendwa wetu. Je! utaenda kwenye arabuni yako?

Bwana na akujaze na furaha ya uwepo wake. Ukamatwe na uamue kukua katika uhusiano wa karibu na Yeye, kwa sababu Neno linasema kwamba wote wantafutao wwatamwona.

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Uchu wa Moyo Wake

Hua wangu, mafichoni mwa jabali, katika stara ya magenge, nitazame uso wako nisikie sauti yako, maana sauti yako ni tamu na uso wako mzuri.

Wimbo Ulio Bora 2:14

Hakuna kitabu kingine kikuu zaidi katika Biblia yote kuhusu uchu wa Bwana kwa ajili ya Bibi arusi Wake kuliko kitabu cha Wimbo Ulio Bora. Katika kitabu hiki, Bwana anaonyesha moyo wake. Hamu yake kwa nyakati zote ni kuwa na Bibi-arusi aliyejitolea ambaye hajachafuliwa na uovu, ni msafi na mtakatifu. Na siku zote ni msafi kwa Yeye kumsafisha ndani yake, yote ni kwa sababu ya njaa yake motomoto kwa ajili Yake.

Bwana-arusi anafurahishwa na wale ambao watakuja Kwake, kwa kuvutiwa na pendo rahisi wanaloshirikiana ne Yeye tu. Huyu ndiye bikira anayemtafuta – Bibi-arusi ambaye hatamwangalia mpenzi mwingine lakini Yeye tu.

Wimbo Ulio Bora 1:2

Kubusu na anibusu kwa kinywa chake maana pambaja zzako zapita divai.

Bibi-arusi Wake anaanza safari ya kumtafuta na hamu. Anamwota mpenzi wake wa kwanza na anakumbuka jinsi ambavyo anamjali kwa kuendelea. Anamtumaini Yeye, na anajifikiria kwa urahisi kuwa katika uwepo

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Wake.Uwepo Wake peke yake unatosheleza hamu yake kwa ajili Yake.

Lakini halafu baada ya muda anatamani zaidi.Bibi-arusi huyu amehisi mikono ya Bwana ikimkumbatia.Amekuwa na nguvu wakati yeye alipojisikia dhaifu.Amekuja karibu sana kando yake akimfariji alipokuwa ameogopa, na alihitaji neno la kutiwa moyo.Lakini bado alikuwa hajawa wake.Alimchukua alipomuhitaji, na kusema asante na akaenda njia yake.Alikuwa bado hajawa Bibi-arusi Wake.

Wimbo Ulio Bora 1:3

Manukato yako yanukia vizuri, jina lako ni kama marhamu iliyomiminwa; kwa hiyo wanawali hukupenda!

Siku ilikuja alipokumbuka zaidi juu ya usikivu wa Bwana.Mawazo yake yakaungana pamoja na Yake, na kwa kadri alivyokaa mahali mahali alipokaa, ndivyo ilivyokuwa zaidi hata kutaja tu kwa jina lake kuliamsha furaha katika moyo wake.

Sasa amefika mahali ambapo amevuka kumwita, akimwomba aje katika maisha yake.Hatamani tena kuendesha maisha yake mwenyewe bali anamwomba afanye hivyo ili ya kwamba atumie muda kwa uranhisi tu kukumbuka minong'ono yake moyoni mwake.Mara wakazoeana.Sasa wamekuwa kila mtu anamtamani mwenzake kwa shauku.Bibi-arusi wake amefika mahali pa kugundua kwamba amechukuliwa kikamilifu na kutaka kuwa pamoja naye wakati wote.

Wimbo Ulio Bora 3:4

Nivute nyuma yako! Na tukimbie Mfalme ameniingiza vyumbani mwake.Tutafurahi na kushangilia; tutanena pambaja zako kuliko divai.

Sasa anatamani sana kuwa na muda pamoja naye, na hili ndilo jambo linaloamsha hamu Yake.Kwa sababu nani awezaye kupinga upendo wa kuendelea wa Bibi-arusi

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

ambaye anazidi kuwa mzuri zaidi, msafi, na anang'aa kwa kila saa ambayo anaitumia kumtafuta Yeye?

Wimbo Ulio Bora 1:5-6

Mimi ni mweusimweusi lakini ninao uzuri, Enyi binti za Yerusalemu, Mfano wa hema za kedari, Kama mapazia yake Sulemani, Msinichunguze kwa kuwa ni mweusimweusi, Kwa sababu jua limeniunguza. Wana wa mamangu walinikasirikia; waliniweka niwe mlinzi wa mashamba ya mizabibu; bali shamba langu mwenyewe sikulilimda.

Bibi –arusi wa Bwana anajua ni mzuri, akisha kutambua hakuna sababu ya kujidharau kama mmoja anayehisi kuhukumiwa au hatoshelezi kwa njia yo yote mbele Yake. Hatakiwi tena kujizingatia mwenye, kutazama mapungufu yake. Bado wala siyo amejiinua kwa sababu ya vipawa na uwezo wake. Badala yake, ana lengo moja tu ambalo linamla mchana na usiku – kuwa pamoja na Bwana-aruis wake mpendwa daima. Haitoshi kuota tu kuwa pamoja naye. Sasa lazima ampate – siyo amiliki tu, bali kuwa nyumbani; siyo kumbadilisha, bali kumpendeza Yeye; siyo kukubalika Naye, bali kujua tayari kwamba anapendeza machoni pake.

Wengi wa marafiki zake na ndugu hapo wanajaribu kumkatisha tamaa asimfuate Mpenzi wake. “Hawezi kujulikana na hawezi kupatikana”, watamwambia, au “Hapana, Yeye hatakiwi kuwa rafiki ambaye anajihusisha na yale unayopenda wewe, kwa sababu ana mambo mengi zaidi ya kufanya kuliko kutumia muda na ndoto zako.”

Wimbo Ulio Bora 1:7

Nijulishe, ee mpendwa wa nafsi yangu, ni wapi ulipolisha kundi lako, ni wapi utakapolilaza adhuhuri, kwa ninikama aliyefungiwa kidoto karibu na makundi ya wenzako?

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Hapana, Amekamatwa kikamilifu na kabisa na usikivu wake, na atapatikana atakapomtafuta, kwa sababu Yeye pia, anafurahishwa na upendo wake.

Je! Wewe ni kama huyu binti, ambaye bila kukoma anamfuatilia mpenzi wake? Je! unakimbia kukimbia kutumia muda pamoja naye paka yake? Huo ndiyo ujumbe wa Bibi rusi ambaye macho yake yanamtazama mchumba wake peke yake. Je! huu ndio uchu wa moyo wako? Humbembeleza Bibi-arusi Wake na uchu mwororo na wa msukumo, na kwa hamu anatarajia kujitoa kwa namna hiyo kwa mioyo yetu tukimrudishia. Kimbia Kwake, na usiruhusu jambo lo lote la maisha haya kuja kati yako na Mpendwa wako! Ni muda gani wa thamani zaidi wa masaa unayotumia katika uwepo Wake uklinywa kutoka kwenye kisima cha uzima wa milele, Yesu Kristo, Chemchemi ya Majai Yaliyo Hai?

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Mwana-Kondoo Atawachunga

Kwa maana huyo Mwana-kondoo aliye katikati ya kiti cha enzi atawachunga, naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai: na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao.

Ufunuo 7:17

Mwana-kondoo ni uzima wetu. Kwa damu yake iliyomwagika kwa ajili yetu, tunaoshwa kuwa safi. Anatupa mavazi mapya ya haki kwa kadri tunavyokaribia kuyapokea. Madhabahu ya ibada ambayo tunairuhusu ikue katika mioyo yetu inakuwa ndiyo inatawala. Tunaruhusu mioyo yetu kupelekwa katika uwepo wake kila tunapotumia muda peke yatu na Mwana-kondoo.

Ufunuo 7:9-10

Baada ya hayo nikaona, na tazama, mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuhesabu, watu wakila taifa na kabila, na jamaa, na ligha, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi, na mbele za Mwana-kondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mtende mikononi mwao; wakilia kwa sauti kuu wakisema, wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi na Mwana-kondoo.

Ufunuo sura ya 7 inianza kwa kuelezea wale watumishi wa Mungu 144, 000 waliopigwa muhuri ambao wanafichwa kutoka kwenye uharibifu. Halafu hali inabadilika katika mstari wa tisa na kwenda kwa watu wengine, wengi sana kutoka kwa kila taifa, jamaa, kabila na lugha ya dunia. Wanasimama mbele za Mwana-kondoo wakiwa wamevikwa mavazi meupe ya haki, na mitende ya ibada

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

mikononi mwao. Kwa sauti wanatangaza sifa na tumaini la wokovu kwa Mwana-kondoo. Ni sura ya ajabu namna gani!

Ufunuo 7:11-13

Na malaika wote walikuwa wakisimama pande zote za kile kiti cha enzi, na za hao wazee, na za wale wenye uhai wane, nao wakaanguka kifulifuli, mbele ya kile kiti cha enzi, wakamsujudu Mungu, wakisema, amina; Baraka na Utukufu na Hekima na Shukrani na Heshima na Uweza na Nguvu zina Mungu wetu hata milele na milele. Amina. Akajibu mmoja wa wale wazee akaniambia, je! watu hawa waliovikwa mavazi meupe ni wakina nani? Nao wametoka wapi?

Wale malaika waliosimama pande zote na biumbe vingine vyote vya kiroho karibu hapo vinaanguka chini katika utisho na ibada. Je! umewahi kufanya hivi katika sehemu yako ya maombi mbele ya Bwana, ukitangaza tabia yake ya ajabu kwa nguvu zako zote?

Halafu swali linakuja, watu hawa ni wakina nani waliovikwa mavazi meupe kutoka kila taifa, kabila, na lugha? Wametoka wapi?

Ufunuo 7:14-17

Nikamwambia, Bwana wangu, wajua wewe. Akaniambia, hao ndio wanatoka katika dhiki ile iliyo kuu, nao wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-kondoo.

Kwa hiyo wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu lake: na Yeye aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema yake juu yao hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena; wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote. Kwa maana huyo Mwana-kondoo aliye katikati ya kiti cha enzi atawachunga, naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao.

Watu hawa wanatoka duniani, wakishaishi katika imani kupitia kwenye dhiki kuu ndani humo. Wapendwa

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

msichanganye hii na ghahdabu ya Mungu ya kutisha inayomwagwa katika dunia na kuonekana katika sehemu nyingine. Ile dhiki kuu hata kama imekuzwa kama dhiki kuu, inafanana na shinikizo la maisha ya hapa duniani. Yesu alitumia neno hilihili kwa wanafunzi wake katika Yohana 16:33: *Hayo nimewaambieni mpate kuwa na amani ndani yangu. Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu.* Alizungumzia juu ya dhiki ikiwa inaongezeka kwa kadri muda unavyoongezeka, ikifanyika kuu nyakati za mwisho, katika Mathayo 24:21 mahali anapowahimiza wote kuvumilia na kubaki waaminifu, licha ya vita, matetesi ya vita, kule kunajisiwa kwa hekalu, n.k.

Hili ndilo jambo lenyewe. Watakatifu wanaosimama mbele ya kiti cha enzi katika mavazi ya haki, wakisha kuayafanya meupe kwa damu ya Mwana-kondoo, ni wale ambao wamekuwa wakinywa kutoka kwenye chemchemi ya maji yaliyo hai muda wote, katika safari yao hadi kwenye kupitia kwenye dhiki ya dunia. *Mtu akiona kiu na aje kwangu anywe²⁴. Walakini yeyote atakayekunywa maji yale nitakayompa mimi, hataona kiu milele; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele²⁵.*

Sasa angalia mstari wa 15 wa Ufunuo 7: *Kwa hiyo wako mbelembele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu lake na Yeye Aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema yake juu yao.*

Marafiki, Yesu akikaa katikati ya watu wake ni uhalisi wa sasa katika Roho. Hii ni kweli leo kwetu tunapoyaruhusu maneno yake kukaa ndani yetu. Yohana 15:7-8 inatambia kwamba *ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu [ufunuo wa rhema] yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtapewa hivyo hutukuzwa Baba yangu, kwa vile mzaavyo sana; nanyi mtakuwa wanafunzi wangu.*

²⁴ Yohana 7:37b

²⁵ Yohana 4:14

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Yesu tayari anaishi katika ya wale ambao husikia sauti ya Bwana! Ni tayari Kristo yuko ndani yao, tumaini la

utukufu. Kama tutaendelea kunywa kutoka kwenye kisima Chake (maneno ambayo anayazungumzia kwenye roho zetu) tunasimama mbele zake tukiwa tumeoshwa safi katika mavazi ya haki! Tunaisikia na kutii sauti, tukimtumikia usiku na mchana. Ni pa utukufu namna gani mahali hapa pa ukaribu na Yeye katika hekalu lake. ni ajabu namna gani unatia nguvu mkate wake kutoka mbinguni, maneno ambayo yanatoka kinywani mwake. Yanaburudisha namna gani maji tunayokunwa kutoka chemchemi ambayo inatiririka kutoka midomoni mwake!

Ufunuo 7:16-17

Hawataona njaa tena wala hawataona kiu tena wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote. Kwa maana huyo Mwana-kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi atawachunga, naye atawaongoza kwenye chemchemi ya maji yenye uhai na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao.

Mwana-kondoo mwenyewe hulichunga kanisa lake. Analisafisha kwa maji ya neno Lake la *rhema*. Yu katikati ya kiti chake cha enzi ambayo sehemu yake ni madhabahu tunayoyatengeneza katika mioyo yetu kwa ajili yake, na kiti cha enzi cha mbinguni ambacho atatukaribisha kukaa pamoja Naye, wale ambao kwa uaminifu wanakunwa kutoka katika chemchemi Yake na kula pamoja naye kusikia sauti Yake²⁶.

Ufunuo 22:1, 16-17

Kisha akanionyesha mto wa maji ya uzima, wenye kung'aa kama bilauri, ukitoka katika kiti cha enzi cha Mungu, na cha Mwana-kondoo.

Mimi Yesu nimmetuma malaika wangu kuwashuhudia ninyi mambo hayo katika makanisa. Mimi ndiye niliye shina na

²⁶ Ufunuo 7:17 inaweza kuonekana ukionyeshwa kupitia Mathayo 4:4, Yohana 10:27, Yohana 14:1-7, Wafeso 5:25-27, Waebrania 12:25-29, na Ufunuo 3:20-21.

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

mzao wa Daudi, ile nyota yenye kung'aa ya asubuhi na Roho na Bibi-arusi wasema, Njoo! Naye asikiaye na aseme, Njoo; Naye mwenye kiu na aje; na yeye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure.

Kwa wengi watoto wa Mungu, maneno haya ya kitabu cha Ufunuo yote ni juu ya wakati uajo. Lakini kwa Bibi-arusi wake ambaye tayari anakunywa kutoka katika mto wa uzima, maneno haya yapo katika wakati uliopo pia. Muda hauna maana mbinguni. Yeye ambaye Kwake siku moja ni kama miaka elfu, na mika elfu moja ni kama siku moja anaangalia tu kwenye maandalizi ya kila mmoja. Je! wanakunywa maji ya kiroho ya kutosha na kula mkate wa uzima wa kiroho wa kutosha? Je! maneno haya ya uzima yako ndani yao? Ni kwa upendo namna gani Mwana-kondoo anatamani kwa ye yote mwenye kiu kuja Kwake na kunywa, na kuwa na ujuzi na kisima cha uzima kinacholeta utukufu wetu wa wakati ujao katika picha ya wakati huu katika Roho. Tunasimama kwa hofu mbele ya kiti Chake cha enzi, tumeoshwa safi, bila doa, kunyanzi, au mawaa kwa sauti yake ambayo inatembea juu ya uso wa maji.

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Basi kwa furaha mtateka maji katika visima vya wokovu

Isaya 12:3

Haya, kila aonaye kiu, njooni majini, naye asiye na fedha; njooni nunueni mle; naam njooni, divai na maziwa, bila fedha na bila thamani, kwani kutoa fedha kwa ajili ya kitu ambacho si chakula na mapato yenu kwa kitu kisichoshibisha? Nisikilizeni kwa bidii, mle kilicho chema, na kujifurahisha nafsi zenu kwa unono. Tegeni masikio yenu na kunijia; sikieni, na nafsi zenu zitaishi, nami nitafanya nanyi agano la milele, naam, rhrma za Daudi zilizo imara. Angalieni, nimemuweka kuwa shahidi kwa kabila za watu; kuwa kiongozi na jemadari kwa kabila za watu. Tazama, utaita taifa usilolijua, na taifa lisilokujua wewe litakukimbilia, kwa sababu ya BWANA, Mungu wako, na kwa ajili yake Mtakatifu wa Israeli; maana amekutukuza. Mtafuteni BWANA, maadamu anapatikana, mwiteni, maadamu yu karibu:

Isaya 55:1-6

Kingdom Faith Ministries International, Inc.

Teaching God's People To Hear His Voice

PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

www.KingdomFaithMinistries.Org

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.